01

## TAARIFA BINAFSI

(I) Jina la Mwanafunzi; NESTORY HANDJON CHILEMEJI
PREM 20120008650

(II) Jina la Mzazi; ESTHER SHADRACK

(III) Kidato ; Kidato cha tatu.

(IV) Anwani ya Posta; 143 BIHARAMULO, KAGERA.

(V) Jina la Shule, Halmashauri ya mkoa.
SHULE YA SEKONDARI BIHARAMULO
KAGERA.

(VI) Anwani ya mkuu wa Shule
- GILBERT BEBWA
- Namba ya Simu; 0621034423

BIHARAMULO SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 143
BIHARAMULO

# MAENDELEO YA TANZANIA BAADA YA UHURU

Maendeleo ni mabadiliko kutoka hali ya chini kwenda hali ya juu katika nyanja mbalimbali. Uhuri ni hali ya kujitegemea na kuwa na maamuzi juu ya jambo fulani. Tanzania ni muunganiko wa Tanganyika na Zanzibar, ambapo nchi hizo ziliungana 26 Aprili 1964. Tanganyika ilipata uhuru 9 Disemba 1961 kutoka kwa waingereza chini ya mwalimu Julius .K. Nyerere na Zanzibar ilipata uhuru 10 Disemba 1963 chini ya Sheikh Abeid Aman Karume. Baada ya uhuru wa nchi hizi mbili ziliweza kuendelea na kubalika kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa na kimichezo ingawa maendeleo hayo Tanzania baada ya uhuru;

Uboreshaji wa huduma za kijamii; Maendeleo ya huduma za kijamii kabla ya uhuru yalikuwa kwa kiwango cha chini kwani vituo vya elimu kama shule zilikuwa chache na hapakuwa na vifaa vya kutosha lakini tu baada ya uhuru shule zimejengwa kila kata na wanafunzi wengi wanahitimu, Pia huduma za afya serikali imejitahidi, kuboresha na kujenga vituo vya afya wilayani na mikoani kwa kiasi kikubwa, Umeme na maji zimeboreshwa kwa kiwango kikubwa, serikali imemtua-Mama wa kitanzania ndoo kichwani na kusambaza huduma ya maji mjini na vijijini hii yote ni kukidhi mahitaji ya watanzania.

Utawala bora na utoaji haki kwa watanzania; Kabla ya uhuru haki za binadamu kwa watanzania zilikuwa

hazizingatiwi kwa usahihi lakini baada ya uhuru Tanzania imefanikiwa kuwa na viongozi waliopatikana kwa mfumo wa Demokrasia na kutoa haki sawa kwa watanzania wote.

Upatikanaji wa fursa za ajira; Kabla ya uhuru watanzania wengi walikuwa hawajaajiliwa na walijikita zaidi kwenye shughuli za kilimo na ufugaji tu. Lakini baada ya uhuru watanzania wameajiriwa katika idara mbalimbali kama vile idara ya elimu, idara ya afya, na idara ya viwanda ajira hizi zimepelekea watanzania wengi kunufaika na mkate wa Taifa.

Uimarishaji wa ulinzi na usalama; Tanzania pia imeimarisha ulinzi na usalama wa watanzania na mali zao kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Jeshi la wananchi (JWTZ) na vyombo vingine vya usalama.

Uhusiano mzuri wa Kimataifa; Tanzania imetengeneza uhusiano na nchi zingine kama China, marekani, Uganda, Kenya kwa ajili ya kudumisha biashara na usafirishaji wa bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine. Pia imejiunga katika mashirika mbalimbali kama Jumuiya ya Afrika mashariki, Jumuhia ya madola mfano uhusiano wa Tanzania na Uganda katika kuanzisha mradi wa bomba la mafuta ambao umewanufaisha wananchi wa pande zote mbili.

Uhimizaji wa kilimo bora; Tanzania imefanikiwa pia kutumia mbinu bora za kilimo kwa kutumia vifaa vilivyo endelea na mbegu bora mfano trekita, plau na mbegu bora kama Jidiko. Pia imetumia mbinu kama umwagiliaji kwa-

ajili ya kuongeza uzalishaji wa malighafi na maendeleo ya Viwanda, kwani kabla ya uhuru watanzania walitumia Vifaa duni kama jembe la mkono na mbegu zisizo bora.

Uboreshaji wa Sekta ya utalii; Kabla ya uhuru nchi ya Tanzania ilikuwa imedolora katika Sekta hii kwani ilikuwa haipewi Kipaumbele, Lakini baada ya uhuru utalii umeboreshwa na kutangaza Soko la utalii ndani na nje ya nchi. Sekta ya utalii imedumisha na kuweka ulinzi mkali katika Vituo au maeneo yenye Vivutio vya utalii mfano Chato Burigi na kuboresha miundombinu na malazi kwenye vivutio hivyo vya utalii.

Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia; Tanzania imeendelea katika Sayansi na Teknolojia kwani baada ya uhuru Vifaa vya Kisayansi kama mashine za X-ray na Vifaa Vingine vinavyotumika hospitalini kama kuongezeka kwa Vitanda vya wagonjwa mfano katika hospitali ya muhimbili aliye kuwa Rais wa Tanzania Hayati Mweshimiwa John Pombe Magufuli aliongeza Vitanda hivyo kwa kiwango kikubwa katika hospitali hiyo pia na hospitali nyingine zilipata ongezeko la Vitanda hivyo. Pia imeendelea katika Swala la mawasiliano, habari zinasambazwa kupitia magazeti, Televisheni. Pia imeboresha Vyombo vya Usafiri kama ndege, daraja la mkapa, daraja la bagamoyo na barabara za juu.

Kutokana na maendeleo hayo Tanzania imefanikiwa kufikia uchumi wa kati yote ni kutokana na jitihada za Viongozi ambao wamekuwa Chachu kuu ya kuhimiza Watanzania kufanya kazi kwa bidii ili kujenga nchi yetu kwani maendeleo yapo kwa watanzania wenyewe.